# Wabunge bora 2025 ‘wachaguliwe’ sasa (2)

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala haya yanayoandikwa na **GABRIEL ISHOLE,** tuliishia sehemu inayomnukuu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akisema kiongozi lazima awe na uwezo wa kifikra unaomtofautisha na watu wengine anaowaongoza. Kwamba, awe na uwezo wa kufikiri kimantiki na kimkakati katika kujieleza kwa ufasaha na kwa ushawishi kuhusu malengo anayotaka yatekelezwe. **ENDELEA...**

HUYU, awe ni mtu aliyeelimishwa vyema, mwenye uwezo wa kutambua mambo mengi ulimwenguni na awe anayejua namna ya kuifanya jamii iendane na mwelekeo wa dunia. Hapa, usomi si tu suala la madarasa mengi shuleni/vyuoni, bali pia uelewa wa mambo aliyojifunza na uzoefu aliojenga katika kazi na majukumu mbalimbali.

Aidha, Mwalimu alieleza uwezo wa kiongozi kuelewa kazi aliyokabidhiwa katika kuongoza kwake. Hapa tunaona kiongozi asiyeelewa kazi aliyopewa ni dhahiri hana uelewa, na kwa kuwa hana uelewa basi pia hawezi kufanya lolote lenye tija kwa wananchi.

Sifa nyingine kwa mujibu wa Nyerere, ni kiongozi kuongozwa na misingi (katiba). Kwamba, kiongozi lazima awe na kitu anachokiamini ambacho ni msingi wa yale anayojaribu kuyatekeleza na akasimamia msimamo wake kwa vitendo na si kwa maneno matupu.

Kwa mfano, mbunge anayo majukumu kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwawakilisha wananchi na kuwasilisha mawazo yao bungeni ili yapatiwe ufumbuzi.

Kwa mtazamo wangu, katika hili wanasiasa wengi hawawatendei haki wananchi kutokana na ukweli kwamba, wanachokwenda nacho bungeni si cha wananchi kwa kuwa wengi hawafanyi mikutano na wananchi kujua kero au mahitaji ya wananchi kwa maana ya kuchukua mawazo na maoni yao ili wayawasilishe bungeni.

Kimsingi, mbunge anapaswa kuwa karibu na wananchi wa jimbo analoliongoza katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Miongoni mwa mambo wanayolalamikiwa wanasiasa wengi hasa wabunge, ni kutokuwa karibu na wananchi baada ya kuchaguliwa kwani wengi ‘hupotea’ na kutoonekana kwa wananchi kana kwamba muda wote wa miaka mitano huwa bungeni.

Wanaofanya hivyo, wanafanya kwa kuwa walipata nafasi hizo kwa njia zisizo halali zinazowafanya wasiwe na wasijione kuwa wanawajibika kwa kuwaongoza na kushirikiana nao kupata maendeleo maana hao wanajua muda ukifika watarudi tena ‘kununua’ kura kwa wajumbe.

Si siri, wananchi wanahitaji viongozi waaminifu wanaoahidi mambo na kuyatimiza kwa kiwango kile kile walichoahidi na kwa wakati sahihi.

Kiongozi lazima awe mwaminifu ili aaminike kwa watu anaowaongoza na ili aaminike, anapaswa kuwa na historia ya kusema ukweli.

Aidha, wananchi wanataka kiongozi anayewasimamia kupata haki wanapoonewa au kutotendewa haki katika shughuli zao za uzalishaji mali na masuala ya kijamii. Kiongozi lazima awe na uwezo wa kutetea na kusimamia haki kwa wote bila upendeleo.

Kwa hiyo, kitu cha kwanza kukisikia wananchi kutoka kwa mgombea wakati wa uchaguzi si nitajenga barabara, au nitajenga zahanati kila kata au nitahakikisha kila mtu ana maji au elimu na vingine. Mambo yote haya ni muhimu lakini si malengo, bali ni njia ya kuyafikia malengo.

Hapa ndipo umuhimu wa elimu unapoonekana maana wanasiasaW wengi wasio na uwezo wamekuwa wakitumia wajibu wa serikali wa kujenga barabara, shule, miundombinu ya umeme na maji kama ndio mitaji na vipaumbele vyao.

Ukiwafuatilia walichokiahidi wakati wa kampeni ni tofauti kabisa na kile wanachokihubiri wakiwa viongozi. Wananchi wanahitaji kiongozi muwazi na mkweli katika vipaumbele vyake.

Kimsingi, mbunge ni mwakilishi na sauti ya wananchi katika Bunge na ikumbukwe katika nchi yetu, anawakilisha hasa jimbo lake ingawa pia masuala ya kitaifa.

Izingatiwe kuwa bunge ndicho chombo kikuu chenye madaraka kwa niaba ya wananchi katika kusimamia na kuishauri serikali na vyombo vyake vyote kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi. Ibara ya 63 (2) na 64 (1) inaelezea vema kazi ya bunge.

Kiuhalisia, mbunge anapaswa kuwa na kazi kuu nne yaani, kuwa kiunganishi cha wananchi au watu wake na serikali pamoja na kupokea ushauri na maoni ya wananchi ili kuyawasilisha katika mamlaka za utekelezaji na kurudisha mrejesho wa hoja na maoni yao.

Nyingine ni kutunga sheria mpya na kufanya marejeo kwa sheria zinazohitaji kurekebishwa au kuboreshwa pamoja na kuishauri na kuikosoa serikali ili iongeze juhudi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mbunge wa jimbo mwenye maono ya kuwatumikia wananchi wake na kuleta maendeleo jimboni kwake hana budi kuwajibika hasa katika naeneo hayo muhimu.

Kufikia malengo na utekelezaji tarajiwa, mbunge makini atafanya utafiti juu ya jimbo lake na kuangalia, kutambua na kubaini changamoto zinazolikabili jimbo na wananchi wake.

Mbunge anayeipenda na kuijua kazi yake, atapaswa kuwa msikivu na anayeheshimu wananchi wake na anayeshirikiana nao katika kazi mbalimbali za kujenga nchi na sambamba na kuleta maendeleo ya jimbo.

Aidha, mbunge (kiongozi) huyo anapaswa kushirikiana na viongozi wa chama na serikali, viongozi wa kiroho au madhehebu ya dini, viongozi wa kimila na asasi za maendeleo katika eneo lake.

Anapaswa kuwa kiungo na msimamizi wa kutetea utawala bora na kuisaidia serikali kuwafikia wanachi katika kubaini na kutatua changamoto zao pamoja na kukusanya maoni ya wananchi na kuhudhuria vikao vya bunge kuyasema yale aliyoambiwa na wananchi wake.

Kutokana na mjadala huo, watu wanapaswa kujiuliza kama hayo ndiyo wanayoyafanya wabunge wetu na kama hawafanyi hivyo, nini kifanyike ili kupata wabunge wenye maono sahihi au kuwashauri waliopo kurejea katika njia sahihi ya kazi na uwajibikaji wa majukumu yao.

Kimsingi, kupata wabunge wanaotakiwa, lazima wananchi waanze sasa ‘kuchagua’ wabunge wao ili kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa 2025 kitakapowadia, wawe walishafanya uchaguzi na sasa wanakwenda kuwaidhinisha kupitia sanduku la kura.

Kwa mujibu wa Ibara ya 63 na Ibara ya 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi za mbunge ni kutunga sheria na kuzisimamia, kushauri serikali na kuridhia mikataba yenye tija kwa taifa.

Kimsingi ninaposikia mbunge anasema maneno kama: ‘…Nitawajengea barabara,’ ‘Nitawajengea shule,’ ‘Nitawajengea hospitali,’ au ‘Nitawachimbia visima…’ na mengine ya namna hiyo, huwa ninapata ukakasi kwa kuwa hawasemi ukweli.

Ni kweli changamoto hizo zipo, lakini mbunge kazi yake ni kuisimamia na kuibana serikali iyatekeleze hayo kwani ni kazi ya serikali sikivu; hapo ndipo huwa anatekeleza wajibu.

Kwa mtazamo wangu, safari hii wanaotaka kugombea ubunge,



waje na hoja za kuuambia umma namna watavyoshiriki kutunga sera na sheria zitakazosaidia kuchochea maendeleo ya wananchi na ustawi wao.

Waliopo madarakani waje watuambie wameisimamiaje serikali na kuishauri kutuletea maendeleo katika jamii na maeneo yetu na hata kiuchumi.

Tusipowasikia bungeni wakishauri sawia uridhiwaji wa mikataba yenye tija na fursa za ajira, basi tujue hawafanyi kazi walizochaguliwa kuzifanya na ndio maana ninasema, “Wabunge bora 2025 ‘wachaguliwe’ sasa.”

**Mwandishi wa makala haya amejitambulisha kuwa ni mdau wa maendeleo Nzega vijijini. Anapatikana kwa 0739200100/0778200100.**

# Wanawake waonesha uwezo katika siasa

**Na Diana Deus**

TANZANIA imeadhimisha Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara huku ikishuhudia uwezo mkubwa wa wanawake katika siasa na uongozi.

Mifano hai, ni uwezo unaooneshwa kwanza, na Rais wa Kwanza mwanamke katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Samia Suluhu Hassan ambaye Watanzania wote wanakiri kuwa, ni mwanasiasa mahiri na kiongozi anayeweza.

Mwingine ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Tulia Ackson, ambaye ameonesha uwezo mkubwa kiungozi ndani na nje ya Tanzania hadi kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani.

Kimsingi, ongezeko la wanawake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024 ni kielelezo cha mwelekeo mzuri na mafanikio ya kisiasa na usawa wa kijinsia nchini katika masuala ya siasa na uongozi.

Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera ni moja ya maeneo nchini yanayoshuhudia ongezeko la wanawake kwenye ngazi ya uongozi wa mitaa kutokana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2024, ikilinganishwa na miaka ya nyuma kutokana na mwitikio wa wanawake waliochaguliwa na waliojitokeza kuwachagua wanawake wenzao.

Wadau mbalimbali likiwamo shirika la kimataifa la FES kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Omuk Hub, Neema Lugangira katika fursa na matukio mbalimbali yakiwamo ya mafunzo, wamekuwa wakisisitiza uthubutu wa wanawake kuwania nafasi mbalimbali katika ngazi ya mitaa, vijiji na halmashauri.

Kwa nyakati tofauti, Lugangira anasema ongezeko la wanawake katika nafasi za uongozi ni ishara ya mafanikio ya sera zinazolenga kuondoa vikwazo vya kijinsia na kuongeza usawa katika maeneo mbalimbali ya jamii.

Kwenye mafunzo yake kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa alisema zipo changamoto zinazowakabili wanawake katika uongozi kwani katika baadhi ya maeneo, wanawake wanakutana na vikwazo vya kijamii, kiuchumi na kimfumo vinavyozuia kushiriki kikamilifu



Wenyeviti wa mitaa katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba wakiwa katika mafunzo kuhusu changamoto na vikwazo vinavyowakabili wanawake kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi. Mafunzo hayo yalitolewa hivi karibuni na shirika la Omuka Hub kwa kushirikiana na shirika la kimataifa la FES Tanzania.

katika siasa na uongozi.

“Hii inaonesha kuwa, licha ya mafanikio bado ipo haja kubwa kuendelea na juhudi za kuvunja mila na desturi ambazo zinawaweka wanawake kwenye nafasi ya chini katika jamii hasa mkoa wangu wa Kagera, lakini naamini kama wanawake watapatiwa nafasi kuna mabadiliko makubwa sana ya kiungozi yatatokea na jamii itajisikia vizuri sana,” anasema.

Wakati wa viapo vyao wenyeviti wa mitaa, taasisi ya Fes Tanzania kwa kushirikiana na mbunge huyo waliwapa mafunzo ya namna ya kutekeleza majukumu yao na umuhimu wa wanawake kuchaguliwa.

Licha ya kushukuru mbunge huyo, wenyeviti hao walimuomba kushiriki mikutano yao ya kwanza ya kupokea kero za wananchi ili aziwasilishe bungeni. Alikiri kupokea mwaliko huo.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, serikali inajitahidi kuhakikisha sera na mikakati yake kuhusu usawa wa kijinsia inatekelezwa na wanawake wanapata fursa sawa katika kila nyanja ya maisha.

Anasema serikali inafanya kila iwezealo kuhakikisha wanawake wanapewa elimu bora, fursa za ajira na kushiriki katika nafasi mbalimbali za siasa na uongozi ukiwamo wa serikali za mitaa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Msimamizi wa Uchaguzi katika Manispaa ya Bukoba, Jacob Nkwera kwa sasa mitaa 12 kati 66 itaongozwa na wanawake ukilinganisha na uchaguzi uliopita wa mwaka 2019 ambao mwanamke mmoja ndiye aliyechaguliwa kuongoza mtaa.

“Tuliwahi kupata mwanamke mmoja na kipindi kingine haikuwa rahisi kumpata… Uchaguzi huu kuna kundi mchanganyiko bado wanawake waliogopa pia kugombea, lakini kwa uchaguzi huu wanawake wameshawishika hapa Bukoba kwani hata kundi mchanganyiko viongozi wanaohitajika ni 198 na kati ya hao 41 ni wanawake hii ni hatua kubwa sana kwetu,” anasema Nkwera.

Anasema wanawake sasa wanashika nafasi zaidi za uongozi katika serikali za mitaa na wengi wao wanachaguliwa kutokana na sifa zao. Hii ni hatua muhimu kwani zamani walikosa nafasi za kuongoza.

Katibu wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) wa Wilaya ya BUKOBA, Rebeca Mkama anasema mabadiliko hayo yanatokana na mikakati ya kutoa nafasi zaidi kwa wanawake katika vyombo vya uongozi, ikiwemo sheria na sera zinazowawezesha wanawake kushiriki katika uchaguzi na mchakato wa kisiasa.

Anasema wanawake wengi wana mtazamo wa karibu na hali halisi ya jamii, hivyo wanaweza kutoa suluhisho bora katika sekta hizi.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza anapongeza vyama vya siasa na wabunge kwa kuendelea kuweka sheria na kufanya mabadiliko makubwa yanayokuza usawa wa kijinsia, hivyo kufanya mpango mzuri wa wanawake kuchaguliwa.

“Wanawake katika uongozi wanachochea usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha kwamba masuala ya wanawake yanapewa kipaumbele,” anasema Nyahoza.

Mkurugenzi wa shirika la kimataifa FES TANZANIA, Christian Denzin anasema, “Kwa kuona wanawake wengine wakiwajibika katika nafasi za juu, wengi zaidi wanaweza kuwa na hamu ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kujiunga na siasa.”

“Hii inaweza kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za ubunge, udiwani na nyingine… Shirika letu linaipongeza Serikali ya Tanzania kwa hatua hii kubwa,” anaongoza.

Mratibu wa shirika la Omuk Hub, Abeid Bushira anasema, “Ingawa kumekuwa na maendeleo, bado kuna tamaduni na imani za kijamii zinazoweka vikwazo kwa wanawake kuchukua nafasi za uongozi, hizi ni pamoja na mifumo ya kijamii inayowaona wanawake kuwa ‘wafuasi’ badala ya ‘viongozi,” anasema Bushira.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyamkazi katika Manispaa ya Bukoba, Crepina Gerazi aliyechaguliwa mwaka huu anasema ukosefu wa rasilimali na mafunzo ni miongoni mwa vikwazo kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika siasa na uongozi.

Anasema, “Kama si hamasa ya Neema Lugangira nisingegombea nakumbuka wanawake wenzangu walinipamba na baadae wakaondoka, wanaume walisema mwanamke hawezi kuamka usiku kukabiliana na changamoto ya ulinzi na usalama…”

Mwenyekiti wa Mtaa wa Miembeni, Ana Ishengoma anasema kuna shinikizo la familia na jamii kwani wanawake wanaoongoza mara nyingi hukutana na shinikizo la kutimiza majukumu ya kifamilia na kijamii, lakini kila jambo hutegemea utaratibu na mipango sawia ili lifanyike sawia.

# Mfumo wa baruapepe na mawasiliano salama serikalini

Inatoka Uk. 9

ama wa mfumo wa GMS, Ndomba anasema mfumo huu umehifadhiwa nchini Tanzania katika mazingira salama.

Aidha, e-GA imeunda timu maalumu inayofanya kazi saa 24 kwa siku kudhibiti matukio hatarishi ya usalama wa mfumo huo na mifumo mingine ya serikali.

Anasema mfumo wa GMS umetengenezwa na vijana wa Kitanzania waliojengewa uwezo na serikali na umezingatia teknolojia ya kisasa.

Kwa mujibu wa Ndomba, mfumo umeisaidia Serikali ya Tanzania kuokoa takribani asilimia 85 ya gharama za uendeshaji ukilinganisha na bei ya soko ya wakandarasi wengine wa nje.

“Mfumo wa GMS hufanyiwa maboresho mara kwa mara kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza ili kudhibiti usalama wa mfumo pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji kwa kuwa, kadri mabadiliko ya teknolojia yanavyojitokeza pia mahitaji ya watumiaji katika mfumo huongezeka na wakati mwingine inatupasa kuongeza ‘features’ (vitu) mpya ili kukidhi mahitaji ya watumiaji,” anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Wahasibu Tanzania (NBAA), Pius Maneno anasema mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa barua ndani ya taasisi za umma.

Anasema awali utumaji wa barua ulikuwa unatumia muda mrefu kufika ofisi iliyokusudiwa na wakati mwingine, barua kufika kwa kuchelewa na kuathiri utekelezaji wake.

“Sasa hivi kupitia GMS kila taasisi imetengenezewa akaunti maalumu kwa ajili ya kutuma barua, hata sisi hapa tuna baruapepe yetu na baada tu ya kubonyeza kitufe cha kutuma, barua hiyo inakuwa imefika sehemu husika bila kuchelewa,” anasema Maneno.

Ofisa Tehama Mwandamizi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Salumu Kulindwa anaipongeza e-GA kwa kutimiza miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa baruapepe serikalini na kuishauri e-GA kuimarisha ushirikiano zaidi kati yake na taasisi nyingine za umma, ikiwemo Costech.

“Katika miaka 10 ya matumizi ya mfumo wa GMS, sisi Costech tunajivunia mfumo huu kwani e-GA imekuwa ikitoa ushirikiano wa haraka pale tunapopata changamoto yoyote katika matumizi ya mfumo huu au hata mfumo mwingine, e-GA hutatua changamoto hizo na kutoa mrejesho kwa wakati,” anasema Kulindwa.

Anaongeza kuwa, Costech imekuwa ikipata ushauri kutoka e-GA kuhusu masuala mbalimbali ya Tehama na hivyo, ushirikiano huo umekuwa chachu kuimarisha matumizi ya Tehama na ujenzi wa serikali mtandao.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano Mwandamizi wa NBAA, Magreth Kageya anasema mfumo wa GMS umerahisisha utumaji na upokeaji wa taarifa za serikali kwa taasisi za umma.

Anasema hii ni kwa kuwa taarifa hizo zinapita mahali salama na hata mpokeaji wa taarifa huwa na uhakika anapokea taarifa kutoka sehemu husika kwa kuwa, baruapepe zote zinakuja na jina la mtumaji, taasisi pamoja na kikoa cha go.tz.

“Kwa sasa usiri na usalama wa taarifa za serikali umeongezeka… Mtumishi anapotuma taarifa zinazohusu serikali, anapata uhakika kuwa taarifa au nyaraka zinapotumwa zinakuwa ni salama na hazitoki nje ya Tanzania na hivyo kudumisha usiri wa taarifa hizo na kulinda maslahi ya taifa letu,” anafafanua Kageya.

Ofisa Utumishi Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Bohari ya Dawa (MSD), Dk Adolar Duwe anasema awali gharama za uendeshaji wa mfumo wa baruapepe katika taasisi za umma zilikuwa kubwa.

Anasema ilipotokea changamoto yoyote ya mfumo, ilibidi kumlipa mkandarasi wa nje aliyejenga mfumo huo ili atatue changamoto husika.

“Uwepo wa mfumo wa GMS umezisaidia taasisi zote zinatumia mfumo huo shirikishi pindi inapotokea changamoto… e-GA huwa inatoa taarifa kwa taasisi zote za umma na changamoto hizo zinatatuliwa bila gharama yoyote na kwa wakati tofauti na awali tulipokuwa tukitumia baruapepe zilizotengenezwa na wakandarasi,” anasema Duwe.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za Tehama wa e-GA, Ricco Boma anasema katika kuhakikisha mfumo wa GMS umehuishwa kutoka GMS 1.0.0 hadi GMS 4.0.0 ili kuuongezea usalama na ufanisi zaidi, umeunganishwa na mifumo mingine ya Tehama ukiwemo mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Uendeshaji wa Shughuli za Taasisi (ERMS) na Mfumo wa Ununuzi (NeST).

Kwa upande wa kuwajengea uwezo maofisa wanaotumia mfumo wa GMS, mkurugenzi huyo anasema mamlaka inatoa mafunzo mbalimbali ya usimamizi wa mfumo kama njia mojawapo ya kuwajengea uwezo maofisa wa vitengo vya Tehama serikalini ili waumudu na kuuendesha mfumo huo kwa ufanisi na ufasaha zaidi.

Meneja wa Huduma za Sheria wa e-GA, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Rafael Rutahiwa anatoa rai kwa watumishi wote wa taasisi za umma, kutumia mfumo wa GMS, kila wanapofanya mawasiliano ya serikali kwani kutokufanya hivyo ni uvunjifu wa Sheria ya Serikali Mtandao Namba 10 ya Mwaka 2019.

Meneja huyo anawataka watumishi wote wanaotumia mfumo wa GMS kuwasilisha changamoto wanazokutana nazo kwa maofisa Tehama wa taasisi zao ili ziwasilishwe katika dawati la msaada wa kiufundi kupitia Mfumo wa Huduma kwa Wateja.